JARIDA LA COPRA

# Thamani

Januari - Juni 2026

## MINYORORO YA THAMANI YENYE USHINDANI KWA USALAMA WA CHAKULA TANZANIA



## DIRA

Kuongoza mageuzi ya Tanzania kuelekea mifumo ya chakula yenye ushindani wa kibiashara, ushirikishwaji na usawa, inayochochea ukuaji wenye manufaa kwa wote.

## DHAMIRA


Kuchochea mageuzi ya minyororo ya thamani ya nafaka na mazao mengine kwa kuimarisha viwango endelevu vya uzalishaji wa kilimo, kukuza uchakataji wa mazao na kuwezesha upatikanaji wa masoko yenye faida yanayoongeza ushindani na kuimarisha usalama wa chakula.





# NGUZO ZA MAADILI

Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao mchanganyiko (COPRA) Itatekeleza Mpango Mkakati wake kwa Kuzingatia Nguzo tano zifuatazo za Maadili:



# Kutoka Dira hadi Sokoni: Kilimo kama nguvu ya uchumi kuelekea 2050

Tanzania inapoelekea mwaka 2050, mjadala kuhusu kilimo hauishii tena katika kuongeza uzalishaji pekee. Hoja kubwa ni namna yakugeuza uzalishaji kuwa usalama wa chakula, biashara, ajira, uwekezaji na ustawi wa Taifa.

Chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, mageuzi ya sekta ya kilimo yameendelea kupewa kipaumbele, kwa kutambua nafasi yake katika kulisha Taifa, kuongeza kipato cha wananchi na kuchochea ukuaji wa biashara na viwanda.

Mwelekeo huo unaakisiwa katika dhamira ya Tanzania kujilisha na kulisha wengine kibiashara, dhana inayoweka uzalishaji wa chakula na biashara katika mkondo mmoja. Tanzania inapozalisha kwa tija na ubora, inalinda usalama wake wa chakula huku ikitumia ziada ya uzalishaji kufungua fursa za masoko ya kikanda na kimataifa.

KILIMO KINACHOONGOZWA NA SOKO

Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 inaweka msisitizo katika kujenga kilimo cha kisasa, chenye tija, kinachotumia teknolojia na kuunganishwa na masoko.
Hivyo, mafanikio ya sekta hayatapimwa kwa kiasi kinachozalishwa pekee, bali pia kwa ubora wa mazao, thamani inayoongezwa, masoko yanayofikiwa na manufaa yanayopatikana kwa wazalishaji na Taifa.

Hii inahitaji mnyororo unaofanya kazi kutoka shambani hadi sokoni, ukiunganisha uzalishaji wenye tija, uhifadhi unaolinda ubora, kupunguza upotevu baada ya mavuno, taarifa sahihi za masoko, biashara yenye ufanisi na uwekezaji katika usindikaji na uongezaji thamani.

Kwa mantiki hiyo, soko linakuwa sehemu ya uamuzi wa uzalishaji, si hatua inayokuja baada ya mavuno. "Tanzania tunayoijenga si ya kuzalisha zaidi pekee, bali ya kuzalisha kwa tija, kuongeza thamani, kujilisha na kulisha wengine kibiashara."

KUTOKA DIRA HADI SOKONI

Katika safari hii, Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA) ina nafasi muhimu ya kusaidia kuunganisha uzalishaji, ubora, biashara na masoko. ina nafasi muhimu ya kusaidia kuunganisha uzalishaji, ubora, biashara na masoko. Kupitia kuimarisha mifumo ya udhibiti, kukuza biashara rasmi na yenye uwazi, kusimamia ubora, kuboresha upatikanaji wa taarifa za masoko na kuhamasisha uongezaji thamani, COPRA inachangia kujenga mazingira ambayo mazao yanakuwa si bidhaa ya shambani pekee, bali rasilimali ya biashara na uwekezaji. Masoko yanapokuwa na ufanisi, ubora ukazingatiwa na wazalishaji wakawa na taarifa sahihi kuhusu mahitaji ya wanunuzi, kilimo kinakuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kuongeza kipato, kuvutia uwekezaji na kuchochea ukuaji wa viwanda.

Kadiri COPRA inavyotekeleza Mpango Mkakati wa 2026/27 hadi 2030/31, mafanikio yake yataonekana si katika udhibiti pekee, bali pia katika namna udhibiti huo unavyosaidia kujenga masoko yenye ushindani, kuongeza thamani na kufungua fursa mpya za biashara.

Hapo ndipo Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 inapogeuka kuwa matokeo yanayoonekana katika mashamba yenye tija, mazao yenye ubora, masoko yenye ushindani, viwanda vinavyoongeza thamani na biashara inayokua.







## Ujumbe wa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi

Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA) ilianzishwa kwa jukumu la kusimamia na kuendeleza biashara ya nafaka na mazao mchanganyiko, kujenga masoko yenye ushirindani na ufanisi, na kuchangia katika kuimarisha usalama wa chakula pamoja na ukuaji endelevu wa uchumi wa Taifa.

Katika kipindi cha miaka miwili na miezi 10 tangu kuanzishwa kwake, COPRA imeweka msingi muhimu wa utekekelezaji wa dhamira yake na kuimarisha nafasi yake katika usimamizi na maendeleo ya sekta. Hatua iliyofikiwa sasa inatoa fursa ya kujenga juu ya msingi huo na kuelekeza nguvu zaidi katika masoko yenye ufanisi na ushindani, uongezaji thamani na ukuaji wa biashara ya mazao.

Kwa Bodi, mafanikio ya COPRA hayapimwi kwa ukuaji wa taasisi pekee, bali kwa matokeo yanayoonekana katika sekta. Tunataka kuona masoko yenye uwazi na ushindani, biashara inayofanyika kwa ufanisi, ongezeko la thamani ya mazao, uwekezaji unaokua na fursa zaidi kwa wakulima, wafanyabiashara, wasindikaji na wadau wengine wa minyororo ya thamani.

Mpango Mkakati wa COPRA wa mwaka 2026/27 hadi 2030/31 unaweka mwelekeo wa hatua inayofuata ya Mamlaka. Jukumu la Bodi ni kuhakikisha COPRA inabaki katika mwelekeo sahihi wa kimkakati, inasimamiwa kwa misingi ya utawala bora na uwajibikaji, na inaendelea kujenga uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya teknolojia, masoko na mazingira ya biashara.

Tunapoangalia miaka mitano ijayo, matarajio yetu ni kuona COPRA ikiwa taasisi imara na yenye kuaminika, inayowezesha masoko kufanya kazi kwa ufanisi na kuchochea ushindani, uongezaji thamani, uwekezaji na ukuaji wa biashara ya nafaka na mazao mchanganyiko nchini.

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, nawapongeza Menejimenti na watumishi wa COPRA kwa kazi iliyofanyika, na kuwashukuru wadau wetu kwa ushirikiano wao katika kipindi cha miaka miwili na zaidi ya safari ya Mamlaka. Bodi itaendelea kutoa uongozi na usimamizi wa kimkakati ili kuhakikisha COPRA inatimiza dhamira yake na kujenga thamani ya kudumu kwa sekta na Taifa.

**Prof. Sifuni Mchome**
**Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mengine (COPRA)**



## Ujumbe wa Mkurugenzi Mkuu

Ni furaha yangu kuwakaribisha katika Thamani, Jarida la COPRA, jukwaa linalosimulia safari ya sekta ya nafaka na mazao mchanganyiko, mafanikio tunayojenga pamoja na fursa zilizopo katika kuongeza thamani ya mazao yetu kuanzia shambani hadi sokoni.

Katika kipindi cha miaka miwili na zaidi tangu kuanzishwa kwa COPRA, tumepiga hatua katika kurasimisha na kukuza biashara ya mazao, kuimarisha mifumo ya masoko, kuboresha upatikanaji wa taarifa na kutumia teknolojia kurahisisha huduma. Lakini nyuma ya mifumo hii kuna jambo muhimu zaidi, thamani tunayojenga kwa wadau tunaowahudumia.

Tunataka kuona mkulima akizalisha kwa tija na kwa kuzingatia mahitaji ya soko, mfanyabiashara akifanya biashara katika mazingira yenye uwazi na ufanisi, msindikaji akipata malighafi yenye ubora, na mwekezaji akiona fursa katika minyororo ya thamani ya mazao. Ndiyo maana tunaangalia safari nzima ya zao, kuanzia uzalishaji na ubora hadi urasimishaji, uongezaji thamani na masoko.

Teknolojia inaendelea kuwa sehemu muhimu ya safari hii. Kupitia COPRA MIS na mifumo mingine ya kidijitali, tunaendelea kurahisisha huduma, kuboresha upatikanaji wa taarifa na kuimarisha usimamizi wa sekta. Sambamba na hilo, tunaendelea kushirikiana na wadau kujenga minyororo ya thamani yenye ushindani na kufungua fursa zaidi za biashara na uwekezaji.

Thamani ni sehemu ya safari hiyo. Kupitia jarida hili tunakuletea mafanikio, fursa, ubunifu na simulizi za wadau wanaochangia mabadiliko katika sekta yetu. Ni nafasi pia ya kujifunza na kuona namna kila mmoja wetu anavyoweza kuchangia katika kuongeza thamani ya mazao ya Tanzania.

Ninawakaribisha kusoma Thamani na kuwa sehemu ya safari ya kujenga sekta ya nafaka na mazao mchanganyiko yenye tija, ushindani na fursa zaidi za biashara.

Thamani ya zao haianzi sokoni, inaanza katika kila hatua ya safari yake.

**Irene Madeje Mlola**
**Mkurugenzi Mkuu**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mengine (COPRA)**





## Ujumbe wa Mkuu wa Kitengo cha Mahusiano ya Umma na Mawasiliano

**Kuunganisha Wadau, Taarifa, Maarifa na Fursa**

Kila mabadiliko huanza na taarifa sahihi. Wakati taarifa zinawafikia watu kwa wakati, zinakuwa maarifa. Maarifa yanapo ongoza maamuzi, huzalisha fursa, huimarisha ushirikiano na kuleta maendeleo.

Ndiyo sababu Thamani limeanzishwa.

Jarida hili ni jukwaa la kuonesha namna sekta ya nafaka na mazao mchanganyiko inavyoendelea kubadilika; kuanzia uzalishaji na uongezaji thamani hadi masoko, uwekezaji, ubunifu na matumizi ya teknolojia. Ni mahali ambapo mafanikio, uzoefu na fursa vinakutana ili kujenga uelewa mpana zaidi wa sekta.

COPRA, tunaamini mawasiliano ni sehemu ya maendeleo. Yanasaidia kuwafikia wakulima kwa taarifa za masoko na uzalishaji, kuwaunganisha wafanyabiashara na fursa za biashara, kuwawezesha wawekezaji kutambua maeneo yenye uwezo wa kukua na kujenga ushirikiano unaohitajika katika kuendeleza sekta.

Ndani ya kurasa hizi utasoma simulizi zinazoonesha jinsi ubora, mifumo ya kidijitali, masoko yaliyopangiliwa, utafiti, uwekezaji na ushirikiano vinavyoendelea kuongeza thamani katika sekta ya nafaka na mazao mchanganyiko. Kila makala imeandaliwa si kwa lengo la kutoa taarifa pekee, bali pia kuchochea mjadala, kubadilishana uzoefu na kufungua mtazamo mpya kuhusu fursa zilizopo.

Jina Thamani limebeba maana kubwa. Linawakilisha thamani ya taarifa sahihi, ya ushirikiano, ya ubunifu na ya kila mdau anayeshiriki katika safari ya kujenga sekta yenye ushindani na inayochangia ustawi wa taifa.

Tunatumaini jarida hili litakuwa daraja la kuunganisha wadau, chanzo cha maarifa na sehemu ya safari ya pamoja ya kuendeleza sekta ya nafaka na mazao mchanganyiko.

Karibu katika toleo la kwanza la Thamani

**Theresia Christian**
**Mkuu wa Kitengo cha Mahusiano ya Umm na Mawasiliano**
**COPRA**

# KUHUSU COPRA

Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA) ni taasisi ya udhibiti iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Usalama wa Chakula, Sura ya 249, yenye jukumu la kusimamia na kuendeleza uzalishaji, uchakataji, uhifadhi, usafirishaji, masoko na biashara ya nafaka na mazao mchanganyiko yanayodhibitiwa nchini Tanzania.

COPRA inalenga kuimarisha mifumo ya chakula na usalama wa chakula nchini, kuboresha na kuweka mifumo rasmi , ya biashara ya mazaokuboresha ubora na ushindani wa mazao katika masoko ya ndani na kimataifa, kuendeleza masoko yenye haki na ufanisi, pamoja na kuweka mazingira wezeshi kwa uwekezaji na ukuaji endelevu wa minyororo ya thamani.

Katika kutekeleza majukumu yake, Mamlaka huandaa na kusimamia mifumo ya udhibiti na viwango vya ubora; husajili na kutoa leseni kwa wadau; hutoa vibali vya kuagiza na kusafirisha mazao nje ya nchi; na kuendeleza masoko rasmi na yenye mifumo iliyopangiliwa. Aidha, COPRA hurahisisha biashara kupitia mifumo ya kidijitali, inakuza kilimo cha mikataba, hutoa taarifa za masoko na kuimarisha uzingatiaji wa sheria, kanuni na viwango katika minyororo ya thamani.

Mamlaka pia inakuza uzalishaji endelevu, upatikanaji na matumizi ya pembejeo bora, usimamizi bora wa mazao baada ya mavuno na maendeleo ya masoko, sambamba na kujenga uwezo wa wakulima, wafanyabiashara na wadau wengine.

Kupitia udhibiti wenye mrengo wa kimaendeleo, mifumo ya kidijitali, ushirikishwaji wa wadau na ushirikiano wa kimkakati, COPRA inaendelea kuendeleza sekta ya nafaka na mazao mchanganyiko iliyorasimishwa, yenye uwazi, inayofuatilika na yenye ushindani wa kibiashara. Dhamira ni kuhakikisha uzalishaji unaunganishwa na masoko, ubora unalindwa katika mnyororo mzima wa thamani na fursa za biashara na uwekezaji zinaongezeka, huku ikiimarisha mifumo ya chakula na usalama wa chakula nchini.



# Nguzo Tano Zinazoongoza Ajenda ya Mageuzi ya COPRA

01 Masoko Yenye Ushindani, Yaliyorasimishwa na Maendeleo ya Biashara za Kilimo na Wanunuzi Wakuu (Off-takers)

02 Wazalishaji na Biashara za Kilimo Zenye Tija, Ustahimilivu na Zilizounganishwa na Masoko

03 Ubora wa Kidijitali na Matumizi ya Takwimu katika Ubunifu wa Mifumo ya Chakula

04 Kuimarisha Utendaji wa Taasisi

05 Mazingira Wezeshi Kupitia Sera, Upatikanaji wa Fedha na Ubia wa Kimkakati




# YALIYOMO


Dira Na Dhamira .......... 2
Nguzo za Maadili.......... 3
Kutoka Dira hadi Sokoni: Kilimo kama nguvu ya uchumi kuelekea 2050.......... 3
Ujumbe wa Mwenyekiti wa Bodi.......... 5
Ujumbe wa Mkurugenzi Mkuu.......... 6
Ujumbe wa Mkuu wa Kitengo cha Mahusiano ya Umma na Mawasiliano.......... 7
Kuhusu COPRA .......... 8

**12**
MASOKO SHINDANI, FURSA ZAIDI
Kuimarisha Biashara na Kufungua Masoko ya Kimataifa

**14**
COPRA MIS: Huduma, masoko na taarifa katika mfumo mmoja

**16**
MBEGU BORA, TIJA ZAIDI
Kuweka msingi wa uzalishaji wenye ubora na ushindani

**18**
KANUNI IMARA, MASOKO IMARA
Kuimarisha Ubora, Usalama Hwa Chakula na Ushindani

**20**
PARACHICHI: THAMANI INAYOKUA
Ubora, masoko na fursa katika mnyororo wa thamani

**22**
KULINDA THAMANI BAADA YA MAVUNO
COPRA Yalenga Kupunguza Upotevu hadi Asilimia 5 Ifikapo 2031

**24**
VIJANA WANAOJENGA KESHO YA KILIMO
Ujuzi, Ajira na Fursa Katika Minyororo ya Thamani


















**26**
KILIMO CHA MKATABA:
Kuzalisha Kukiwa na soko

**28**
THAMANI INAYOVUKA MIPAKA
Safari ya Ufuta wa Tanzania KUuelekea Masoko ya Dunia

# Kuimarisha Biashara na Kufungua Masoko ya Kimataifa

Katika mwaka 2024/25, Tanzania ilisafirisha tani milioni 1.99 za nafaka na mazao mchanganyiko zenye thamani ya TZS trilioni 6.32 kupitia mazao yanayosimamiwa na COPRA. Takwimu hizi zinaakisi mchango unaozidi kuongezeka wa biashara ya mazao katika uchumi wa Taifa, huku zikionesha fursa zinazopanuka kwa wakulima, wafanyabiashara, wachakataji na wasafirishaji katika masoko ya kikanda na kimataifa.

Mafanikio haya yanakwenda sambamba na juhudi za Serikali za kufanya kilimo kuwa biashara, kupanua wigo wa masoko ya kikanda na kimataifa na kujenga mifumo ya biashara iliyorasimishwa, yenye uwazi na ushindani.

Kwa COPRA, kujenga masoko hayo ni muhimu ili kuhakikisha ongezeko la uzalishaji linatafsiriwa kuwa thamani kubwa zaidi kwa wakulima, wafanyabiashara, wachakataji, wasafirishaji na uchumi kwa ujumla.

“Naiona COPRA kama moja ya taasisi zinazotafsiri Mpango Kabambe wa Kilimo 2050 kuwa matokeo yanayoonekana na kuchangia kufikiwa kwa matarajio ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050,” anasema Mkurugenzi Mkuu wa COPRA, Bi. Irene Madeje Mlola.

**Kuunganisha uzalishaji na masoko**

Tanzania ina uwezo mkubwa wa uzalishaji, lakini kupata thamani kamili ya uwezo huo kunahitaji zaidi ya kuzalisha kwa wingi. Masoko ya uhakika, ubora wa mazao, ufuatiliaji katika mnyororo wa thamani, mifumo bora ya baada ya mavuno, taarifa sahihi za masoko na uzingatiaji wa matakwa ya biashara ndani na nje ya nchi ni miongoni mwa mambo yanayoamua ushindani wa mazao.

COPRA inaendelea kuimarisha maeneo haya kupitia mifumo ya leseni na vibali vya kuagiza na kusafirisha mazao nje ya nchi, kuendeleza masoko rasmi na yenye mifumo iliyopangiliwa, kukuza kilimo cha mikataba, kuimarisha udhibiti wa ubora na kusajili wadau katika minyororo ya thamani. Mifumo ya kidijitali nayo inaongeza ufanisi na uwazi wa biashara, huku ikiimarisha upatikanaji wa taarifa za masoko, ufuatiliaji wa mazao na usimamizi wa shughuli za sekta.

Juhudi hizi zinaenda sambamba na kukuza uzalishaji endelevu, kuongeza upatikanaji wa mbegu bora, kuboresha usimamizi wa mazao baada ya mavuno na kuimarisha uwezo wa kitaalamu katika minyororo ya thamani inayodhibitiwa.

Lengo ni kujenga mazingira ambayo uzalishaji unaongozwa zaidi na mahitaji ya soko, huku wakulima na wafanyabiashara wakiwa na uwezo wa kushindana katika masoko ya ndani na kimataifa.



Ms. Irene Madeje Mlola
Director General



“Mikakati yetu inalenga kuifanya kilimo kuwa biashara kwa kupanua fursa katika masoko ya kikanda na kimataifa, kuongeza thamani ya mazao na kuinua kipato cha wakulima kupitia biashara yenye ushindani,” anasema Bi. Mlola.

**Kupanua wigo wa masoko ya nje**

Katika mwaka 2024/25, kiasi cha nafaka na mazao mchanganyiko kilichosafirishwa nje ya nchi kilifikia tani milioni 1.99, kutoka tani milioni 1.75 mwaka uliotangulia, sawa na ongezeko la takribani asilimia 14. Thamani ya mauzo hayo iliongezeka kutoka TZS trilioni 6.06 hadi TZS trilioni 6.32.

Hadi kufikia Machi 2026, tani milioni 1.58 zenye thamani ya TZS trilioni 4.1 zilikuwa tayari zimesafirishwa nje ya nchi katika mwaka 2025/26, ikiashiria kuendelea kwa shughuli za mauzo katika masoko ya kimataifa.

Mauzo hayo yanajumuisha wigo mpana wa mazao, yakiwemo nafaka, mikunde, mbegu za mafuta, mazao ya bustani, matunda na viungo. Ufuta, mahindi, mchele, mbaazi, parachichi, kakao na maharage ni miongoni mwa mazao yanayoonesha ukubwa na utofauti wa fursa zilizopo katika minyororo ya thamani nchini.

Utofauti huu una umuhimu mkubwa katika kujenga biashara yenye uwezo wa kuhimili mabadiliko ya masoko, huku ukifungua fursa kwa wazalishaji kutoka maeneo na minyororo tofauti ya mazao.

**Masoko yanayoongeza thamani**

Umuhimu wa mauzo ya nje hauishii kwenye thamani ya mazao yanayovuka mipaka. Biashara ya mazao inachochea shughuli mbalimbali katika mnyororo wa thamani, kuanzia uzalishaji na ukusanyaji hadi uhifadhi, uchakataji, usafirishaji na huduma za kifedha.

“Kila tani inayosafirishwa nje ya nchi inawakilisha fursa ya kipato kwa mkulima, mahitaji zaidi ya huduma za usafirishaji na ugavi, fursa kwa waendeshaji wa maghala, wachakataji na wasafirishaji, pamoja na biashara zaidi kwa taasisi za fedha zinazowezesha minyororo ya thamani,” anasema Bi. Mlola.

Masoko rasmi na yenye mifumo iliyopangiliwa yana nafasi muhimu katika kuhakikisha wakulima wanashiriki na kunufaika zaidi na ukuaji huu. Upatikanaji wa taarifa sahihi za bei na mahitaji ya soko, mifumo ya biashara yenye uwazi, viwango vya ubora vinavyoeleweka na uhusiano bora na wanunuzi vinaongeza uwezo wa mkulima kufanya maamuzi ya kibiashara na kupata thamani stahiki ya mazao yake.

Urasimishaji wa biashara pia unaimarisha mahusiano kati ya wazalishaji, wachakataji, wasafirishaji, taasisi za fedha na wawekezaji, hatua muhimu katika kuifanya kilimo kuwa biashara yenye tija na ushindani.

**Ubora: ufunguo wa masoko ya kimataifa**

Kadiri mahitaji ya masoko ya kimataifa yanavyobadilika, ushindani hautategemea wingi wa mazao pekee. Ubora, uthabiti wa bidhaa, ufuatiliaji wa chanzo, uzalishaji endelevu na uwezo wa kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa kwa uhakika vinazidi kuwa vigezo muhimu vya biashara.

COPRA inaendelea kuimarisha mifumo ya udhibiti, ubora na masoko ili kusaidia wadau kukidhi matakwa hayo, huku biashara ya mazao ikifanyika kwa ufanisi na katika mazingira yanayotabirika.

“Kadiri uzalishaji unavyoongezeka, viwango vya ubora vinavyoimarika na uwekezaji katika uongezaji thamani unavyopanuka, Tanzania inazidi kujijengea nafasi ya kuwa msambazaji wa kuaminika wa mazao katika masoko ya Afrika, Asia, Ulaya na Mashariki ya Kati,” anasema Bi. Mlola.

Mwelekeo huu unaendana na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, Mpango Kabambe wa Kilimo 2050 na Ajenda 10/30 Kilimo Ni Biashara, ambazo zinaweka msisitizo katika biashara ya kilimo, uongezaji thamani, maendeleo ya masoko na kuongeza ushiriki wa Tanzania katika biashara ya kikanda na kimataifa.

Fursa iliyopo sasa ni kuunganisha uzalishaji na masoko kwa ufanisi zaidi, kuongeza thamani inayobaki nchini na kuwezesha wakulima na wafanyabiashara kushindana katika masoko ambayo ubora, uaminifu na uhakika wa bidhaa vina thamani kubwa.

Kwa COPRA, kujenga masoko yaliyorasimishwa, yenye mifumo iliyopangiliwa na ushindani ni msingi wa kuunganisha uzalishaji na biashara, kuongeza thamani ya mazao na kufungua fursa zaidi kwa wakulima, wafanyabiashara na uchumi wa Tanzania kwa ujumla.

# COPRA MIS:
# Huduma, masoko na taarifa katika mfumo mmoja

COPRA inaendelea kujenga mfumo wa kidijitali unaounganisha huduma za udhibiti, taarifa za masoko na biashara ya nafaka na mazao mengine kupitia Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa wa COPRA (COPRA MIS). Mfumo huu unalenga kurahisisha huduma kwa wadau, kuimarisha usimamizi wa sekta na kuwezesha maamuzi yanayotegemea taarifa sahihi na zinazopatikana kwa wakati.

COPRA MIS inaunganisha huduma ambazo awali zingeweza kutekelezwa kupitia mifumo au taratibu tofauti zenye kumlazimu mdau kutuma barua au kufika ofisini. Usajili wa wadau, utoaji wa leseni na vibali, ufuatiliaji wa uzingatiaji wa sheria na kanuni, pamoja na taarifa za masoko na takwimu za udhibiti, vinawekwa katika mazingira yaliyounganishwa ya kidijitali.

Kwa wadau, mabadiliko haya yanamaanisha kupata huduma kwa urahisi zaidi, kufuata taratibu za udhibiti kwa uwazi na kupata taarifa muhimu kwa shughuli zao za biashara. Kwa COPRA, mfumo unatoa uwezo mpana zaidi wa kuona mwenendo katika minyororo ya thamani, kufuatilia uzingatiaji wa matakwa ya kisheria na kiudhibiti, na kutumia takwimu katika kupanga, kusimamia na kufanya maamuzi.






Afisa Kilimo wa COPRA Kanda ya Mashariki Abubakar Mzanda akitoa maelezo ya huduma zinazotolewa na Mamlaka kwenye Maonesho ya Sabasaba

Hivyo, mageuzi haya hayaishii katika kuhamisha huduma kutoka kwenye makaratasi kwenda mtandaoni. Yanajenga muunganiko kati ya mdhibiti, wadau na masoko, huku taarifa zikifanya kazi kama kiungo muhimu katika kuongeza uwazi, ufuatiliaji na ufanisi wa sekta.

Mwelekeo huu wa kidijitali unaonekana pia katika biashara ya mazao. Mwaka 2025, zaidi ya kilo milioni 713.6 za mazao zenye thamani ya zaidi ya TZS trilioni 1.4 ziliuzwa kupitia minada ya kidijitali. Kiasi kilichouzwa kiliongezeka kwa asilimia 166 ikilinganishwa na mwaka 2024, ikiashiria kuongezeka kwa matumizi ya mifumo rasmi ya kidijitali katika biashara ya mazao.

"COPRA MIS inabadilisha namna tunavyounganisha udhibiti, masoko na taarifa. Kwa kuleta huduma na takwimu katika mfumo mmoja uliounganishwa, tunaongeza uwazi na ufanisi, huku tukipata uwezo mkubwa zaidi wa kufuatilia na kusimamia minyororo ya thamani inayoendelea kubadilika," anasema James Mtatifikolo, Mkuu wa Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, COPRA.

Kadiri COPRA MIS inavyoendelea kuimarishwa, matarajio ni kuwa na mazingira ambayo mdau anaweza kupata huduma za udhibiti kwa njia rahisi zaidi, taarifa muhimu zinaweza kuunganishwa na kutumika kwa ufanisi, na Mamlaka inaweza kufuatilia shughuli katika minyororo ya thamani kwa usahihi zaidi.

Hatua hii inaweka msingi wa sekta iliyorasimishwa, inayofuatilika, yenye uwazi na inayotumia taarifa kufanya maamuzi, huku COPRA ikiwa na nyenzo imara zaidi za kusimamia masoko yanayokua na kuwa na ushindani zaidi.

**COPRA MIS inabadilisha namna tunavyounganisha udhibiti, masoko na taarifa. Kwa kuleta huduma na takwimu katika mfumo mmoja uliounganishwa, tunaongeza uwazi na ufanisi, huku tukipata uwezo mkubwa zaidi wa kufuatilia na kusimamia minyororo ya thamani inayoendelea kubadilika.**



James Mtatifikolo, Mkuu wa Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano wa COPRA

MBEGU BORA, TIJA ZAIDI

# Kuweka msingi wa uzalishaji wenye ubora na ushindani





**Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Mhe. Mboni Mhita akipokea kutoka kwa Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa COPRA Bw. Kalvin Remen na Mkurugenzi Mkuu wa COPRA Bi. Irene Mlola sehemu ya mbegu bora iliyotolewa na COPRA wakati wa uzinduzi wa zoezi la kugawa mbegu kwa wakulima ili kupunguza uhaba wa mbegu bora kwa wakulima.**

Zaidi ya wakulima 43,000 katika mikoa 23 wamenufaika na mpango wa Serikali wa usambazaji wa mbegu zilizothibitishwa unaotekelezwa kupitia COPRA, hatua inayopanua upatikanaji wa mbegu bora kwa lengo la kuongeza tija, kuboresha ubora wa mazao na kuongeza kipato cha wakulima.

Hadi kufikia Juni 2026, COPRA ilikuwa imenunua na kusambaza tani 164.024 za mbegu zilizothibitishwa zenye thamani ya TZS bilioni 1.12 kwa wakulima 43,299 katika mamlaka 92 za serikali za mitaa. Mbegu hizo zilihusisha ufuta, mbaazi, dengu, choroko, alizeti na soya, mazao yenye umuhimu katika usalama wa chakula, masoko ya ndani na biashara ya mazao.

Usambazaji wa mbegu umeenda sambamba na kuimarisha huduma za kitaalamu kwa wakulima. Jumla ya maafisa ugani 3,365 wamepatiwa mafunzo rejea kuhusu Kanuni Bora za Kilimo, Good Agricultural Practices, ili kuongeza uwezo wao wa kuwasaidia wakulima kutumia mbinu bora za uzalishaji, usimamizi wa mazao na teknolojia za kisasa.

"Kuongeza tija kunaanzia katika kuhakikisha wakulima wanapata pembejeo bora za uzalishaji. COPRA tunawekeza katika mbegu bora, miche iliyothibitishwa na mifumo endelevu ya uzalishaji kwa sababu ndiyo msingi wa kuimarisha usalama wa chakula, kuongeza kipato cha wakulima na kujenga sekta yenye ushindani," anasema Mkurugenzi Mkuu wa COPRA, Bi. Irene Madeje Mlola.

**Kupanua fursa katika mazao yenye thamani kubwa**

Juhudi za COPRA hazijaishia kwenye mbegu pekee. Mamlaka pia inapanua upatikanaji wa miche bora ya mazao yenye thamani kubwa kama parachichi, kakao na viungo, ili kuwawezesha wazalishaji kunufaika na fursa zinazokua katika masoko ya ndani na nje ya nchi.
Katika utekelezaji huo, miche 129,986 ya parachichi pamoja na miche 58,190 ya kakao na viungo imesambazwa kwa wakulima. Upatikanaji wa miche bora una umuhimu katika kuongeza tija, kujenga uthabiti wa ubora wa mazao na kuwawezesha wazalishaji kukidhi mahitaji ya masoko yanayozidi kuhitaji viwango vya juu.

Kwa kupanua upatikanaji wa mbegu na miche bora, COPRA inaweka msingi wa uzalishaji wenye tija, ubora na uwezo mkubwa zaidi wa kuunganishwa na fursa za kibiashara.

**Kupanua wigo mwaka 2026/27**

Baada ya hatua zilizofikiwa, COPRA inalenga kupanua zaidi upatikanaji wa mbegu na miche bora katika mwaka wa fedha 2026/27.

Mamlaka imepanga kununua na kusambaza tani 600 za mbegu zilizothibitishwa za ufuta, mbaazi, alizeti, choroko, dengu na soya. Aidha, tani 20.3 za mbegu za awali zitanunuliwa kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania, TARI, ili kusaidia wazalishaji wa Mbegu za Ubora Uliotangazwa, QDS, na kuongeza upatikanaji wa mbegu bora zinazozalishwa nchini.

COPRA pia imepanga kununua na kusambaza miche bora milioni 1.6 ya kakao, viungo, parachichi na tufaha.

Upanuzi huu utaenda sambamba na kuimarisha maarifa ya uzalishaji. Jumla ya wakufunzi 5,440 wanatarajiwa kujengewa uwezo kuhusu Kanuni Bora za Kilimo, wakiwemo maafisa ugani 2,590 na wakulima viongozi 2,850 katika kanda zote saba za COPRA.

"Tumeweka kipaumbele katika mbegu bora, miche bora na mafunzo ya Kanuni Bora za Kilimo kwa sababu ni msingi wa kuongeza tija, kuboresha ubora wa mazao na kuimarisha ushindani katika masoko ya ndani na kimataifa," anasema Pendo Bigambo, Kaimu Mkurugenzi wa Uendelezaji Mazao na Uwekaji Viwango, COPRA.

Kwa kuunganisha upatikanaji wa mbegu na miche bora na huduma imara za ugani, COPRA inaendelea kuweka msingi wa tija kubwa, mazao yenye ubora na ushiriki mpana wa wakulima katika masoko. Upanuzi uliopangwa mwaka 2026/27 unalenga kufikisha fursa hizi kwa wakulima wengi zaidi na kuimarisha minyororo ya thamani ya mazao ya kimkakati nchini.



**Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mazao na Viwango wa COPRA Bi. Pendo Bigambo akiwa na Mkuu wa Kanda ya Mashariki Bi. Mary Majule wakikagua shehena ya mbegu iliyoandaliwa na ASA kwa ajili ya kuisambaz na kuwagawia wakulima kwenye maeneo mbalimbali.**





## KANUNI IMARA, MASOKO IMARA

# Kuimarisha Ubora, Usalama wa Chakula na Ushindani

Hatua muhimu imefikiwa katika kuimarisha mfumo wa usimamizi wa sekta ya nafaka na mazao mchanganyiko baada ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali kwa kanuni nne zilizotungwa chini ya Sheria ya Usalama wa Chakula, Sura ya 249.

Kanuni hizo zinahusu udhibiti wa ubora wa nafaka na mazao mchanganyiko, usimamizi wa mafuta ya kula, usimamizi wa zao la parachichi na kilimo cha mikataba. Kwa pamoja, zinaweka msingi wa kuimarisha usalama na ubora wa chakula, kuendeleza uzalishaji endelevu, kurasimisha biashara na kujenga masoko yenye uwazi na ushindani.

Kwa COPRA, kanuni hizi zinaimarisha mifumo inayosimamia mazao kuanzia uzalishaji hadi sokoni. Zinaboresha viwango vya ubora, usimamizi baada ya mavuno, uhifadhi wa mazao, ufuatiliaji wa bidhaa, uwazi katika biashara na uzingatiaji wa matakwa ya masoko, hatua zinazochangia kulinda mlaji na kuongeza ushindani wa mazao ya Tanzania.

"Kanuni bora zinaweka msingi wa kuhakikisha ubora na usalama wa mazao vinazingatiwa katika kila hatua ya mnyororo wa thamani. Hili linaimarisha imani ya walaji, linaongeza ushindani wa mazao yetu na kujenga mazingira bora ya biashara," anasema Kamwesige Mtembei, Mkurugenzi wa Uendelezaji Mazao na Uwekaji Viwango, COPRA.

**Kuweka kanuni kwenye vitendo**

Mbali na kutunga kanuni, COPRA inaendelea kuziunganisha na utekelezaji wa vitendo katika minyororo ya thamani ya mazao yanayodhibitiwa.

Mamlaka imeandaa miongozo 16 ya uzalishaji endelevu kwa mazao mbalimbali, pamoja na miongozo ya masoko na viwango vitatu vya kitaifa vya uzalishaji endelevu. Hatua hizi zinasaidia kuboresha ubora wa mazao, usalama wa chakula, ulinzi wa mazingira na utayari wa bidhaa kuingia katika masoko ya ndani na kimataifa.

Ili kuhakikisha utekelezaji wake unakuwa na matokeo, maafisa ugani 3,006, wakiwemo vijana 425 kupitia programu ya Building a Better Tomorrow (BBT), wamepatiwa mafunzo kuhusu viwango vya uzalishaji endelevu na Kanuni Bora za Kilimo.

Aidha, maafisa 22 wamejengewa uwezo kuhusu mahitaji ya ukaguzi kwa mujibu wa kiwango cha ISO/IEC 17020, huku maafisa wengine 21 wakipatiwa mafunzo kuhusu uthibitishaji wa GLOBALG.A.P. COPRA pia imenunua seti 64 za vifaa vya ukaguzi wa ubora wa mazao ili kuimarisha ukaguzi katika masoko na maeneo ya biashara.



Kaimu Mkuu wa COPRA Kanda ya Ziwa Bw. Timotheo Chillewa akiongoza timu ya wataalamu kwenye zoezi la kukagua hali ya maghala kabla ya kuanza kwa minada ya zao la mbaazi katika mikoa ya kanda hiyo

Katika mnyororo wa thamani wa parachichi, wavunaji 484 wamepatiwa mafunzo kuhusu uvunaji sahihi na usimamizi baada ya mavuno, huku maafisa ugani 104 wakijengewa uwezo katika usimamizi wa ubora wa minyororo ya thamani ya parachichi na mikunde. Hatua hizi zinaimarisha uzingatiaji wa ubora, ufuatiliaji wa mazao, utunzaji sahihi na uwezo wa kukidhi mahitaji ya masoko.

Kwa upande wa kilimo cha mikataba, kanuni mpya zinaweka mfumo rasmi wa mahusiano kati ya wazalishaji, wanunuzi, wachakataji, wawekezaji na taasisi za fedha. Mfumo huu unarahisisha upatikanaji wa pembejeo, huduma za kitaalamu, mitaji na masoko, huku ukiimarisha uwazi na kulinda maslahi ya wazalishaji.

**Kujenga imani katika masoko**

Kwa kuunganisha mfumo wa kanuni na utekelezaji wake, COPRA inaendelea kujenga mazingira yanayowezesha upatikanaji wa chakula salama, masoko yanayofanya kazi kwa ufanisi na mazao yenye ushindani mkubwa zaidi.

Hatua hizi zinaweka msingi wa mifumo ya chakula iliyo imara, biashara yenye uwazi na mazao yanayoweza kushindana katika masoko ya ndani na kimataifa, huku zikichangia usalama wa chakula na maendeleo endelevu ya sekta ya kilimo nchini.

# Ubora, masoko na fursa katika mnyororo wa thamani

Parachichi linazidi kujijengea nafasi miongoni mwa mazao yenye thamani kubwa nchini Tanzania, likifungua fursa kwa wakulima, wasafirishaji, wachakataji na biashara mbalimbali zinazohudumia mnyororo wake wa thamani.

Ukuaji wa mahitaji katika masoko ya ndani na kimataifa unafanya zao la parachichi kuvuka mipaka ya uzalishaji pekee. Ubora wa miche, utaalamu katika uzalishaji na uvunaji, usimamizi bora baada ya mavuno, ukusanyaji wa mazao, uchakataji na maandalizi kwa ajili ya soko vinazidi kuwa muhimu katika kuongeza thamani ya zao hili.

COPRA inaunga mkono ukuaji huu kwa kuimarisha hatua mbalimbali za mnyororo wa thamani, kuanzia upatikanaji wa miche bora na maarifa ya kitaalamu hadi miundombinu ya baada ya mavuno, usimamizi wa ubora na maendeleo ya masoko.

"Fursa iliyopo kwenye parachichi haiishii katika kuongeza uzalishaji. Tunahitaji kujenga mnyororo wa thamani wenye uwezo wa kutoa kwa uthabiti ubora unaohitajika na masoko, huku ukiongeza thamani ya kibiashara kwa wakulima na wafanyabiashara," anasema Lilian Mpinga, Mkuu wa Kitengo cha Mazao ya Bustani na Pareto, COPRA.

**Ubora unaanzia shambani**

Ubora wa parachichi unaanzia kwenye miche bora na usimamizi sahihi wa uzalishaji. COPRA imesambaza zaidi ya miche 89,285 ya parachichi kwa wazalishaji, ikiwa ni sehemu ya juhudi za kuongeza upatikanaji wa miche bora, kuimarisha uzalishaji na kuweka msingi wa bustani zenye tija zinazoweza kukidhi mahitaji ya soko.

Sambamba na usambazaji wa miche, COPRA imewekeza katika kuimarisha ujuzi wa uvunaji na utunzaji wa zao. Jumla ya wavunaji 266 wa parachichi, wakiwemo vijana chini ya programu ya Building a Better Tomorrow (BBT), wamepatiwa mafunzo maalumu kuhusu mbinu bora za uvunaji, utunzaji wa matunda na usimamizi wa ubora.

Kwa zao la parachichi, ubora unaojengwa shambani unahitaji kulindwa katika hatua zote zinazofuata. Namna tunda linavyovunwa, kutunzwa na kuandaliwa kwa ajili ya soko inaweza kuathiri ubora wake na hatimaye thamani yake ya kibiashara.

Fursa hiyo inaonekana pia katika mauzo ya nje. Mauzo ya parachichi yaliongezeka kutoka tani 35,627 zenye thamani ya TZS 252.3 mwaka 2023/24 hadi tani 37,871 mwaka 2024/25 zenye thamani ya TZS bilioni 267.2, ikiashiria kuendelea kwa mahitaji ya parachichi la Tanzania katika masoko ya kimataifa.

Mbali na soko la parachichi bichi, uzalishaji wa mafuta ya parachichi unafungua fursa zaidi za uchakataji, uongezaji thamani na kupanua wigo wa bidhaa zinazoweza kufikia masoko ya ndani na kimataifa.

**Thamani baada ya mavuno**

Kadiri uzalishaji unavyopanuka, umuhimu wa kile kinachotokea baada ya parachichi kuvunwa nao unaongezeka. Ubora unaopatikana shambani unahitaji kulindwa katika ukusanyaji, utunzaji, usafirishaji na maandalizi ya zao kwa ajili ya soko. COPRA inawezesha uendelezaji wa vituo 20 vya ukusanyaji wa parachichi na mazao ya bustani katika mikoa ya Mbeya, Njombe, Iringa, Ruvuma na Rukwa. Miundombinu hii inalenga kuboresha ukusanyaji na utunzaji wa mazao karibu na maeneo ya uzalishaji, hatua muhimu katika kupunguza upotevu na kuhifadhi ubora kabla ya mazao kufikishwa sokoni.

Aidha, kituo cha kisasa cha kufungasha parachichi, packhouse, katika UWAMARU AMCOS, Wilaya ya Rungwe, kinaendelezwa kupitia ubia kati ya sekta ya umma na binafsi. Kituo hicho kitaimarisha upangaji wa madaraja, uchambuzi, ufungashaji na maandalizi ya parachichi kwa ajili ya masoko ya ndani na nje ya nchi.

> Fursa iliyopo kwenye parachichi haiishii katika kuongeza uzalishaji. Tunahitaji kujenga mnyororo wa thamani wenye uwezo wa kutoa kwa uthabiti ubora unaohitajika na masoko, huku ukiongeza thamani ya kibiashara kwa wakulima na wafanyabiashara.



Lilian Mpinga, Mkuu wa Kitengo cha Mazao ya Bustani na Pareto COPRA.



Uwekezaji huu unaimarisha kiungo kati ya bustani na masoko kwa kusaidia kuhifadhi ubora na kuhakikisha zao linaandaliwa kulingana na mahitaji ya wanunuzi.

COPRA pia imeandaa mwongozo wa uzalishaji endelevu wa parachichi, sambamba na mfumo wa kanuni za usimamizi wa zao hilo. Hatua hizi zinaweka msingi wa kuimarisha uzalishaji bora, ufuatiliaji, usimamizi baada ya mavuno na uzingatiaji wa matakwa ya soko katika mnyororo wa thamani.

**Fursa iliyo mbele**

Kupitia Mpango Kabambe wa Kilimo 2050, Tanzania inalenga kuongeza uzalishaji wa parachichi kutoka tani 190,648 hadi tani 243,000 ifikapo mwaka 2030, huku tija ikitarajiwa kuongezeka kutoka tani nane hadi tani tisa kwa hekta.

Ukuaji huu unafungua fursa zinazokwenda mbali zaidi ya kuongeza uzalishaji. Vitalu vya miche, vituo vya ukusanyaji, vituo vya kufungasha, uchakataji, ufungashaji, usafirishaji, huduma za kitaalamu na biashara ya nje vinaweza kuwa maeneo muhimu ya uwekezaji na biashara kadiri mnyororo wa thamani unavyoendelea kukua.

Fursa iliyopo sasa ni kuunganisha hatua hizi kwa ufanisi zaidi, kuanzia miche na uzalishaji bora, kulinda ubora wakati wa uvunaji na baada ya mavuno, hadi uchakataji na kufikia masoko yenye thamani kubwa.

Hatua inayofuata katika ukuaji wa parachichi haitapimwa kwa wingi wa matunda yanayozalishwa pekee, bali pia kwa thamani inayoongezwa kutoka shambani hadi sokoni na fursa za biashara zinazojengwa katika kila hatua ya mnyororo wa thamani.

# COPRA Yalenga Kupunguza Upotevu hadi Asilimia 5 Ifikapo 2031

COPRA imeweka lengo la kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno kutoka asilimia 35 hadi asilimia 5 ifikapo Juni 2031, ikiwa ni sehemu ya juhudi za kulinda chakula kinachozalishwa, kuhifadhi ubora wa mazao na kuongeza thamani inayopatikana kwa wakulima na wafanyabiashara.

Lengo hilo, lililowekwa katika Mpango Mkakati wa COPRA wa mwaka 2026/27 hadi 2030/31, linaenda sambamba na azma ya kuongeza thamani ya nafaka na mazao mchanganyiko yaliyochakatwa kutoka dola za Marekani bilioni 1.5 hadi bilioni 3 katika kipindi hicho kama inavyobainishwa pia kwenye Mpango Kabambe wa Mageuzi ya Kilimo 2050. Hii inaweka usimamizi wa mazao baada ya mavuno na uongezaji thamani miongoni mwa maeneo muhimu katika mwelekeo wa Mamlaka.

Upotevu baada ya mavuno bado ni changamoto kubwa. Makadirio yanaonesha kuwa kati ya asilimia 15 na 20 ya nafaka na mikunde hupotea baada ya mavuno, huku kiwango hicho kikifikia hadi asilimia 40 kwa mazao ya bustani. Hasara hii haipunguzi tu kiasi cha chakula kinachopatikana, bali pia huathiri kipato cha wakulima, ubora wa mazao na kiasi kinachoweza kuingia kwenye uchakataji na biashara.

**Kulinda kilichozalishwa**

COPRA inakabiliana na changamoto hii kupitia uwekezaji katika miundombinu ya baada ya mavuno, uboreshaji wa mbinu za utunzaji wa mazao na kuimarisha mifumo inayolinda ubora kutoka shambani hadi sokoni.

Hadi sasa, miundombinu 197 ya baada ya mavuno imeanzishwa katika maeneo muhimu ya uzalishaji. Miundombinu hiyo inajumuisha vituo 106 vya kukaushia pareto, vituo 20 vya ukusanyaji wa parachichi na mazao ya bustani, vituo saba vya kukaushia kakao na vituo 20 vya kuchakata vanila. Aidha, kituo cha kisasa cha kufungasha parachichi kinaendelezwa kupitia ubia kati ya sekta ya umma na binafsi.

Uwekezaji huu unazingatia mahitaji tofauti ya kila mnyororo wa thamani. Vituo vya ukusanyaji vinawezesha mazao ya parachichi na bustani kukusanywa na kutunzwa vizuri zaidi, huku vituo vya ukaushaji vikisaidia kuhifadhi ubora wa pareto na kakao. Vituo vya vanila vinaongeza uwezo wa kuchakata zao hilo na kuwezesha thamani zaidi kupatikana kabla ya bidhaa kufika sokoni.

Katika mnyororo wa thamani wa parachichi, vituo 20 katika mikoa ya Mbeya, Njombe, Iringa, Ruvuma na Rukwa vinaimarisha uwezo wa kukusanya na kutunza mazao karibu na maeneo ya uzalishaji. Hatua hii inaenda sambamba na uendelezaji wa kituo cha kisasa cha kufungasha parachichi katika UWAMARU AMCOS, Wilaya ya Rungwe, kitakachosaidia upangaji wa madaraja, uchambuzi, ufungashaji na maandalizi ya mazao kwa ajili ya masoko ya ndani na nje ya nchi.

Miundombinu hiyo inaenda sambamba na kuimarisha ujuzi katika hatua za uvunaji na utunzaji. COPRA imewapatia mafunzo wavunaji 266 wa parachichi, wakiwemo maafisa ugani vijana 50 chini ya programu ya Building a Better Tomorrow, kuhusu mbinu za uvunaji na utunzaji zinazolenga kupunguza uharibifu wa matunda na kuhifadhi ubora.

**Kutoka upotevu hadi thamani**

Kupunguza upotevu baada ya mavuno si suala la kuzuia mazao yasiharibike pekee. Uvunaji sahihi, ukaushaji, uhifadhi, ukusanyaji, utunzaji na uchakataji vina maana kwamba sehemu kubwa zaidi ya kile kinachozalishwa inaweza kuhifadhi ubora wake, kufika sokoni na kuendelea kuzalisha thamani katika mnyororo.

Ifikapo Juni 2031, COPRA inalenga kupunguza upotevu baada ya mavuno katika nafaka lengwa, mbegu za mafuta na mikunde hadi asilimia 5. Kwa mazao ya bustani, viungo na mazao ya mizizi, ambayo upotevu unaweza kufikia asilimia 40, lengo pia ni kufikia asilimia 5.

Sambamba na hilo, lengo la kuongeza thamani ya nafaka na mazao mengine yaliyochakatwa kutoka dola za Marekani bilioni 1.5 hadi bilioni 3 linaonesha mwelekeo mpana zaidi wa kuhakikisha thamani zaidi inapatikana baada ya uzalishaji kupitia utunzaji bora, uchakataji na maandalizi ya mazao kwa ajili ya soko.

Kufikia lengo la kupunguza upotevu kutoka asilimia 35 hadi asilimia 5 kutamaanisha sehemu kubwa zaidi ya mazao yanayozalishwa na wakulima inafika kwa walaji, wachakataji na masoko. Hii itaongeza thamani inayopatikana kutokana na uzalishaji, kuboresha fursa za kipato na kuchangia upatikanaji wa chakula na usalama wa chakula nchini.

Kwa COPRA, kuongeza uzalishaji ni muhimu, lakini kulinda kile ambacho tayari kimezalishwa ni sehemu muhimu ya kuhakikisha uzalishaji huo unageuka kuwa thamani.







Wafanyakazi wa Mamlaka ua Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko wakiwahudumia wadau waliotembelea banda la maonesho la COPRA wakati wa Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika kitaifa kwenye viwanja vya Chinangali, Jijini Dodoma.



# Ujuzi, Ajira na Fursa katika minyororo ya thamani



Vijana wa Mradi wa Jenga Kesho Iliyo Bora (BBT) unaoendeshwa na Wizara ya Kilimo wakiwa kazini.

Vijana wanaendelea kuwa nguvu muhimu katika mageuzi ya sekta ya kilimo nchini. Kupitia uwekezaji katika ujuzi, uzoefu wa vitendo na ajira, COPRA inaendelea kufungua fursa zinazowawezesha kushiriki kikamilifu katika minyororo ya thamani ya nafaka na mazao mchanganyiko.

Kupitia programu mbalimbali, Mamlaka imewajengea uwezo maafisa ugani 3,365 na kuchangia kuanzishwa kwa ajira za moja kwa moja 855, hatua zinazoonesha kuwa maendeleo ya sekta ya kilimo yanazalisha fursa zinazokwenda mbali zaidi ya uzalishaji wa shambani.

Miongoni mwa waliopata mafunzo ni vijana 425 kupitia programu ya Serikali ya Building a Better Tomorrow (BBT), ambao wamejengewa uwezo katika teknolojia za kisasa za uzalishaji, Kanuni Bora za Kilimo, usimamizi wa ubora na kilimo kinachozingatia mahitaji ya soko.

Kupitia programu hiyo, COPRA iliwapeleka waatalamu wa kilimo vijana 50, wakiwemo wanaume 26 na wanawake 24, katika mikoa ya Njombe, Mbeya, Songwe, Iringa, Rukwa na Ruvuma ili kusaidia maendeleo ya mnyororo wa thamani wa parachichi. Wakifanya kazi bega kwa bega na wakulima, vijana hao wanachangia kuboresha uzalishaji, usimamizi wa ubora na uzingatiaji wa viwango vinavyohitajika katika masoko yenye thamani kubwa.

Mbali na kuongeza uwezo wa wakulima, programu hiyo imewapa vijana uzoefu wa vitendo katika taaluma za ugani, agronomia na kilimo cha kibiashara, huku ikiongeza wataalamu wenye ujuzi katika sekta ya kilimo.


FURSA KATIKA KILA HATUA YA MNYORORO WA THAMANI

Fursa za ajira kwa vijana zimeendelea kujitokeza pia kupitia shughuli za usajili wa wakulima na usimamizi wa mazao baada ya mavuno.

Usajili wa wakulima wa kakao, parachichi na ngano ulihusisha vijana 581, wakiwemo wanaume 391 na wanawake 190 katika mikoa ya Mbeya, Morogoro, Tanga na Manyara. Mbali na kuimarisha mifumo ya taarifa za wakulima, zoezi hilo limefungua nafasi katika ukusanyaji wa takwimu, uhamasishaji wa wakulima na usimamizi wa taarifa za kilimo.

Katika mnyororo wa thamani wa parachichi, juhudi za kuboresha uvunaji zimezalisha fursa kwa vijana na wanawake 216, wakiwemo wanaume 153 na wanawake 63 katika mikoa ya Njombe na Mbeya. Washiriki walipatiwa mafunzo kuhusu mbinu sahihi za uvunaji zinazosaidia kupunguza uharibifu wa mazao, kuhifadhi ubora wa matunda na kuongeza uwezo wa kukidhi mahitaji ya soko.

Aidha, vijana wengine wanane walipata fursa katika uzalishaji wa miche bora ya parachichi, hatua inayodhihirisha kuwa ajira zinaendelea kujitokeza katika maeneo mbalimbali ya mnyororo wa thamani.




Hatua hizi zinaonesha kuwa kilimo cha kisasa kinahitaji zaidi ya uzalishaji. Kimefungua nafasi katika ugani, agronomia, usimamizi wa taarifa, uzalishaji wa miche, usimamizi baada ya mavuno, huduma za masoko na shughuli nyingine zinazounga mkono maendeleo ya sekta.

Kwa kuwekeza katika ujuzi na kuwapa vijana fursa za kujifunza na kufanya kazi katika mazingira halisi ya biashara ya kilimo, COPRA inaendelea kuchangia azma ya Serikali ya kujenga sekta ya kilimo yenye tija, ushindani na fursa nyingi za ajira na ujasiriamali kwa kizazi cha sasa na kijacho.




Picha ya pamoja ya wakufunzi, viongozi na washiriki wa mafunzo elekezi kwa vijana wa BBT-Ugani yaliyoendeshwa na COPRA mkoani Iringa ikiwa ni juhudi za Mamlaka kuongeza nguvu za wataalamu wa ugani kwenye zao la parachichi. Vijana hao walisambazwa kutoa usaidizi wa ugani kwenye wilaya zinazolima parachichi mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

## KILIMO CHA MKATABA:

# Kuzalisha ukiwa na soko

Kwa mkulima, mafanikio hayaishii kwenye mavuno mengi pekee. Kujua soko linahitaji nini, nani atanunua mazao, ubora unaotakiwa na masharti ya biashara ni mambo yenye umuhimu sawa na uzalishaji wenyewe.

Kwa mkulima, mavuno mazuri ni sehemu moja tu ya biashara. Kufahamu soko linahitaji nini, nani atanunua, ubora unaotakiwa na masharti ya biashara ni muhimu katika kuhakikisha uzalishaji unaleta matokeo ya kibiashara.

Kilimo cha mikataba ni mfumo wa masoko unaounganisha uzalishaji na soko kupitia makubaliano rasmi kati ya wazalishaji na wanunuzi, wachakataji, wawekezaji au washirika wengine wa kibiashara. Mfumo huu unamwezesha mkulima kupanga uzalishaji kwa kuzingatia mahitaji ya soko, huku wanunuzi wakipata uhakika zaidi wa kiasi na ubora wa mazao wanayohitaji.

Kwa mujibu wa Kamwesige Mtembei, Mkurugenzi wa Uendeshaji na Udhibiti Ubora wa COPRA, kuimarisha uhusiano huu ni muhimu katika kuelekeza uzalishaji kwenye biashara inayozingatia mahitaji ya soko.

"Kilimo cha mikataba kinamwezesha mkulima kuzalisha akiwa na uelewa wa soko analolenga. Mzalishaji anapofahamu mahitaji ya mnunuzi kabla ya kuanza uzalishaji, anakuwa katika nafasi nzuri ya kuamua nini azalishe, ubora unaohitajika na namna ya kuandaa mazao yake kwa ajili ya soko," anasema Mtembei.

**Kujenga uelewa kwa mahusiano bora ya kibiashara**

COPRA inaendelea kuongeza uelewa wa kilimo cha mikataba miongoni mwa wazalishaji na wadau wengine wa soko. Hadi sasa, Mamlaka imetoa mafunzo kwa wadau 996, wakiwemo wakulima, wafanyabiashara, wachakataji na wanunuzi katika mikoa saba.

Mafunzo hayo yamewafikia wadau 452 Geita, 145 Mbeya, 120 Tabora, 112 Katavi, 91 Rukwa, 70 Kigoma na sita Dodoma. Kupitia mafunzo hayo, wadau wamejengewa uelewa kuhusu namna kilimo cha mikataba kinavyofanya kazi, pamoja na wajibu wa kila upande katika makubaliano ya kibiashara.

Kwa wazalishaji, kilimo cha mikataba kinaweza kuongeza uhakika wa soko na, kulingana na makubaliano yaliyopo, kurahisisha upatikanaji wa pembejeo bora, huduma za kitaalamu, ugani na fedha. Kwa upande mwingine, wanunuzi na wachakataji wanaweza kupata mazao kwa kuzingatia kiasi, ubora na muda wa uwasilishaji uliokubaliwa, hivyo kuwawezesha kupanga ununuzi na shughuli zao za biashara kwa ufanisi zaidi.

"Kilimo cha mikataba kinakuwa na matokeo mazuri pale pande zote zinapoelewa uhusiano wa kibiashara unaowaunganisha. Mkulima anapaswa kuelewa soko na wajibu wake, na mnunuzi pia anapaswa kutekeleza masharti yaliyokubaliwa na kujenga uhusiano unaozalisha thamani kwa pande zote," anasema Mtembei.



"

**Kilimo cha mikataba kinamwezesha mkulima kuzalisha akiwa na uelewa wa soko analolenga. Mzalishaji anapofahamu mahitaji ya mnunuzi kabla ya kuanza uzalishaji, anakuwa katika nafasi nzuri ya kuamua nini azalishe, ubora unaohitajika na namna ya kuandaa mazao yake kwa ajili ya soko.**

Mkurugenzi wa Oparesheni na Udhibiti Ubora - COPRA





Wakulima, wavunaji na wafanyabiashara wa zao la parachichi Mkoa wa Arusha wakipatiwa mafunzo kwa vitendo kuhusu uvunaji sahihi na matunzo ya zao hilo ili kupunguza upotevu wa mazao unaosababishwa na uangalizi usio sahihi unaofanywa wakati na baada ya mavuno.

**Kuimarisha mfumo wa kilimo cha mikataba**

Kanuni za Usalama wa Chakula za Kilimo cha Mikataba za mwaka 2026 zinaweka mfumo rasmi wa kusimamia mahusiano ya kilimo cha mikataba. Mfumo huo unajumuisha uhakiki na usajili wa mikataba na COPRA, ufuatiliaji wa utekelezaji wa makubaliano, pamoja na taratibu za utatuzi wa migogoro na ulinzi wa maslahi ya wazalishaji.

Hatua hii inafanya kilimo cha mikataba kuwa zaidi ya makubaliano ya kuuza mazao baada ya mavuno. Ni mfumo unaounganisha maamuzi ya uzalishaji na mahitaji ya soko, huku ukiweka msingi wa mahusiano ya kibiashara yenye uwazi, uwajibikaji na manufaa kwa pande zinazoshiriki.

Kwa kuunganisha mafunzo kwa wadau na mfumo ulio wazi wa kisheria, COPRA inaendelea kuimarisha kilimo cha mikataba kama mfumo wa masoko unaomwezesha mkulima kuanza uzalishaji akiwa tayari analitazama soko, huku wanunuzi wakijenga vyanzo vya uhakika na endelevu vya mazao.




## THAMANI INAYOVUKA MIPAKA

# Safari ya Ufuta wa Tanzania kuelekea masoko ya dunia

Ukuaji wa mnyororo wa thamani wa ufuta unaonekana katika kuongezeka kwa mahitaji ya zao hili katika masoko ya ndani na kimataifa. Leo, ufuta ni miongoni mwa mazao muhimu ya biashara ya nje ya Tanzania, ukiendelea kuchangia mapato ya mauzo ya nje na kufungua fursa kwa wakulima, wafanyabiashara, wachakataji na wasafirishaji.

Mafanikio haya hayaakisi ongezeko la biashara pekee, bali yanaonesha maendeleo ya mnyororo wa thamani wa ufuta, kuanzia uzalishaji na ubora wa zao hadi mifumo ya masoko na biashara inayozidi kuimarika.

"Ufuta unaonyesha wazi kile kinachowezekana pale uzalishaji wenye ubora unapounganishwa na masoko yaliyorasimishwa na mahitaji ya uhakika.

Dhamira yetu ni kuendelea kuimarisha mnyororo mzima wa thamani ili wakulima wanufaike zaidi, huku Tanzania ikiendelea kujenga nafasi yake katika biashara ya kimataifa," anasema Mkurugenzi Mkuu wa COPRA, Bi. Irene Madeje Mlola.

**Kuimarisha msingi wa uzalishaji**

Mnyororo imara wa thamani wa ufuta unaanzia shambani. Upatikanaji wa mbegu bora na matumizi ya mbinu bora za uzalishaji vinawawezesha wakulima kuongeza tija na kuzalisha ufuta unaokidhi mahitaji ya soko.

COPRA imesambaza tani 38 za mbegu bora zilizothibitishwa za ufuta, sambamba na kuandaa miongozo ya uzalishaji endelevu na kutoa mafunzo ya Kanuni Bora za Kilimo kwa maafisa ugani na wakulima. Hatua hizi zinaimarisha huduma za ugani, kuongeza tija na kuhakikisha ubora wa zao unaanza kujengwa tangu shambani.

Kwa zao linalolenga zaidi masoko ya nje, msingi huu ni muhimu. Ukuaji wa biashara ya ufuta hautategemea kuongeza uzalishaji pekee, bali pia uwezo wa kuzalisha kwa ubora unaokidhi mahitaji ya wanunuzi.

**Kuimarisha masoko yaliyorasimishwa**

Kadiri uzalishaji unavyoongezeka, ndivyo umuhimu wa masoko yaliyorasimishwa unavyozidi kuongezeka.

Mwaka 2025, kilo milioni 223 za ufuta zenye thamani ya TZS bilioni 623.3 ziliuzwa kupitia minada ya kidijitali, ikilinganishwa na kilo milioni 144.3 mwaka 2024. Hii inaakisi juhudi za Mamlaka katika kupanua wigo wa maeneo yanayozalisha zao hili kuingia kwenye mfumo huu.

Minada ya kidijitali imeendelea kujenga mazingira ya biashara yenye uwazi, ushindani na ugunduzi wa bei unaozingatia nguvu ya soko. Wakati huohuo, mifumo hiyo imeimarisha uhusiano kati ya wazalishaji, wanunuzi na wasafirishaji kwa kuweka biashara katika mazingira rasmi na yanayotabirika zaidi.

Kwa wakulima, hatua hii inaongeza upatikanaji wa taarifa za soko na uelewa wa mahitaji ya wanunuzi. Kwa wafanyabiashara na wasafirishaji, inawezesha upatikanaji wa mazao kwa utaratibu unaoaminika na kujenga mahusiano ya muda mrefu katika biashara.

**Ubora kuimarisha ushindani**

Kadiri biashara ya ufuta inavyopanuka, umuhimu wa ubora unaendelea kuongezeka.

COPRA imeandaa miongozo ya uzalishaji na masoko ya ufuta inayounganisha mbinu bora za uzalishaji na mahitaji ya soko. Sambamba na hilo, hatua za kuboresha utunzaji wa mazao, uhifadhi, ukusanyaji na uzingatiaji wa viwango vya ubora zinaendelea kulinda thamani ya zao tangu shambani hadi sokoni.

"Ushindani katika masoko ya kimataifa haujengwi kwa kuongeza uzalishaji pekee. Wanunuzi wanahitaji ubora, uthabiti na uhakika wa bidhaa. Kuimarisha maeneo haya katika kila hatua ya mnyororo wa thamani ndiyo msingi wa kuendeleza biashara ya ufuta ya Tanzania," anasema Bi. Mlola.

**Kufungua thamani zaidi**

Zao la ufuta linaonesha ukubwa wa mchango wa zao hili katika biashara ya nje na uchumi wa Tanzania.

Hata hivyo, fursa iliyopo haiishii katika kuongeza kiasi cha ufuta kinachosafirishwa nje ya nchi.

Uwekezaji zaidi katika usafishaji, upangaji wa madaraja, uchakataji, ufungashaji na shughuli nyingine za uongezaji thamani unaweza kuongeza sehemu ya thamani inayobaki nchini kabla ya zao kufika katika masoko ya kimataifa. Hii itafungua fursa mpya kwa wachakataji, wawekezaji na biashara nyingine zinazohudumia mnyororo wa thamani wa ufuta.

**Mnyororo wa thamani unaokua**

Maendeleo ya mnyororo wa thamani wa ufuta yanaonesha mabadiliko makubwa yanayotokea katika sekta. Kutoka katika uzalishaji unaolenga kuuza mazao ghafi, Tanzania inaendelea kujenga mfumo unaounganisha uzalishaji wenye ubora, masoko yaliyorasimishwa, uongezaji thamani na biashara ya kimataifa.

Hatua zilizofikiwa tayari zinaonekana. Wakulima wanapata mbegu bora na huduma za ugani, biashara ya ufuta kupitia minada ya kidijitali inaendelea kukua, na mauzo ya nje pia yanaendelea kuongezeka.

Hatua inayofuata ni kuimarisha ubora, kupanua uchakataji na uongezaji thamani, kuendelea kuunganisha wazalishaji na masoko na kuhakikisha sehemu kubwa zaidi ya thamani inayotokana na biashara ya ufuta inabaki nchini.

Kwa kufanya hivyo, ufuta unaendelea kujidhihirisha si kama zao la biashara pekee, bali kama mnyororo wa thamani unaochochea biashara, uwekezaji na ukuaji wa uchumi wa Tanzania.



# Mikunde; Uchumi na thamani inayokua



Mikunde imeendelea kuwa zaidi ya mazao ya chakula. Leo, mazao kama mbaazi, maharage, dengu, choroko na soya yanazidi kuwa nguzo muhimu ya biashara ya kilimo, yakichangia ukuaji wa uchumi, kuongeza mapato ya wakulima na kupanua fursa za biashara ndani na nje ya nchi.

Mabadiliko hayo yanaonekana wazi katika biashara ya mbaazi. Katika mwaka mmoja pekee, zao hili liliingiza takribani TZS bilioni 824.98 kupitia mauzo ya nje, na kulifanya kuwa zao linaloongoza kwa thamani ya mauzo ya mikunde kutoka Tanzania.

Ukuaji huu unaashiria mabadiliko makubwa katika sekta. Mikunde haipimwi tena kwa kiasi kinachozalishwa pekee, bali kwa thamani inayozalishwa katika kila hatua ya mnyororo wa thamani, kuanzia shambani, kupitia biashara na uchakataji, hadi kufikia masoko ya ndani na kimataifa.

**Kujenga msingi wa uzalishaji**

Kadiri mahitaji ya soko yanavyoendelea kuongezeka, uzalishaji wa mikunde unahitaji kuendana na ubora, tija na matarajio ya wanunuzi.
Katika kuimarisha msingi huo, COPRA imeendelea kuboresha upatikanaji wa mbegu bora, kuandaa miongozo ya uzalishaji endelevu na kujenga uwezo wa wakulima pamoja na maafisa ugani kuhusu Kanuni Bora za Kilimo. Hatua hizi zinaimarisha uzalishaji wenye tija, kuboresha ubora wa mazao na kuwawezesha wazalishaji kuzalisha kwa kuzingatia mahitaji ya soko.

Kwa kufanya hivyo, msingi unawekwa wa kukidhi mahitaji yanayoongezeka katika masoko ya ndani na yale ya kimataifa.

**Masoko yaliyorasimishwa yafungua fursa**

Ukuaji wa sekta ya mikunde unaonekana pia katika namna biashara inavyofanyika.

Biashara ya mbaazi kupitia minada ya kidijitali iliongezeka kutoka kilo milioni 95.5 hadi zaidi ya kilo milioni 301.4, huku biashara ya dengu ikiongezeka kutoka kilo milioni 21.5 hadi karibu kilo milioni 147.

Ongezeko hili linaonesha kuimarika kwa matumizi ya mifumo rasmi ya biashara inayowaunganisha wazalishaji na wanunuzi katika mazingira yenye uwazi zaidi, ushindani wa haki na ugunduzi sahihi wa bei.



Sambamba na hilo, kilimo cha mikataba kinaendelea kujenga daraja kati ya uzalishaji na soko kwa kuwaunganisha wakulima na wanunuzi kupitia makubaliano yanayoeleza kiasi cha mazao, ubora unaohitajika na masharti ya biashara. Mfumo huu unamwezesha mkulima kuzalisha akiwa na uelewa wa mahitaji ya soko, huku wanunuzi wakipata uhakika wa upatikanaji wa mazao yanayokidhi mahitaji yao.

Kwa pamoja, mifumo hii inaendelea kuunganisha uzalishaji na mahitaji ya soko, na kujenga mazingira bora zaidi ya biashara kwa mazao ya mikunde.

**Kukidhi mahitaji ya masoko ya kimataifa**

Masoko ya kimataifa yanaendelea kuwa kichocheo muhimu cha ukuaji wa sekta ya mikunde, hususan kwa zao la mbaazi.

India inaendelea kuwa miongoni mwa masoko makubwa ya mbaazi za Tanzania. Kuendelea kwa msamaha wa ushuru wa forodha kwa uagizaji wa mbaazi nchini India kumeendelea kufungua fursa muhimu kwa wakulima, wafanyabiashara na wasafirishaji wa Tanzania.

Mapato ya mauzo ya nje ya mbaazi yaliyofikia takribani TZS bilioni 824.98 yanaonesha uwezo mkubwa uliopo pale uzalishaji wa ndani unapounganishwa na mahitaji ya masoko ya kimataifa.

Hata hivyo, kudumisha mafanikio hayo kutategemea uwezo wa kuzalisha mazao yenye ubora unaokidhi viwango vya soko, kuhakikisha upatikanaji wa mazao kwa wakati na kujibu mahitaji yanayobadilika ya wanunuzi.

**Kuongeza thamani katika mnyororo wa thamani**

Kadiri uzalishaji na biashara vinavyoendelea kukua, fursa kubwa zaidi ipo katika kuongeza thamani kabla mazao hayajafika kwa mlaji wa mwisho.

Ukusanyaji wa mazao, uhifadhi, usafishaji, upangaji wa madaraja, uchakataji, ufungashaji na huduma za usafirishaji ni maeneo yanayofungua nafasi mpya za biashara na uwekezaji, huku



yakiongeza thamani ya mazao yanayozalishwa na wakulima.

Uchakataji, hususan, una nafasi kubwa ya kupanua wigo wa bidhaa zinazotokana na mikunde, kufungua masoko mapya, kuvutia uwekezaji na kuhakikisha sehemu kubwa zaidi ya thamani inayotokana na mazao haya inabaki nchini.

Kupitia Mpango Kabambe wa Kilimo 2050, Tanzania inalenga kuongeza uzalishaji wa mbaazi hadi tani 400,000 ifikapo mwaka 2030, huku uzalishaji wa maharage ukitarajiwa kufikia tani milioni 2.3. Uzalishaji wa soya na choroko unatarajiwa kufikia tani 200,000 na tani 205,000 mtawalia.

Kadiri minyororo hii ya thamani inavyoendelea kukua, lengo si kuongeza uzalishaji na biashara pekee, bali kujenga uchumi wa mikunde unaounganisha uzalishaji wenye tija, masoko yaliyorasimishwa na biashara yenye ushindani, huku ukizalisha thamani kubwa zaidi kwa wakulima, wafanyabiashara na uchumi wa Tanzania kwa ujumla.



# Mahitaji viuatilifu hai, fursa uwekezaji Pareto



Sekta ya pareto nchini Tanzania inaonesha fursa kubwa kwa wakulima, wachakataji na wawekezaji, huku mahitaji ya maua makavu ya pareto yakiwa juu ya uzalishaji wa sasa kwa zaidi ya tani 5,000 kwa mwaka.

Kwa sasa, Tanzania inazalisha takribani tani 4,000 za maua makavu ya pareto kwa mwaka, wakati viwanda vya uchakataji vinahitaji takribani tani 9,000. Pengo hili linaonesha nafasi kubwa ya kuongeza uzalishaji, kuimarisha upatikanaji wa malighafi nchini na kuvutia uwekezaji katika hatua mbalimbali za mnyororo wa thamani.

Kwa COPRA, hii ni fursa ya soko iliyo wazi. Mahitaji yapo, lakini uzalishaji bado haujafikia kiwango kinachohitajika na wachakataji.

"Pareto ni zaidi ya zao la biashara la jadi. Tayari kuna mahitaji ambayo uzalishaji wa sasa hauwezi kuyakidhi, hali inayofungua fursa kwa wakulima, vijana na wawekezaji kushiriki katika mnyororo huu wa thamani," anasema Lilian Mpinga, Mkuu wa Kitengo cha Mazao ya Bustani na Pareto, COPRA.

Pareto ina thamani kutokana na pyrethrins, viambato asili vya sumu vinavyopatikana katika maua yaliyokaushwa na kutumika katika utengenezaji wa bidhaa za kudhibiti wadudu. Kuongezeka kwa matumizi ya bidhaa za kudhibiti wadudu zinazotokana na vyanzo vya asili kunapanua fursa ya kibiashara kwa nchi zinazozalisha pareto, ikiwemo Tanzania.

Uzalishaji wa pareto umejikita zaidi katika maeneo ya nyanda za juu ya Mbeya, Songwe, Njombe, Iringa, Manyara na Arusha, ambako hali ya hewa inafaa kwa zao hilo. Kwa sasa, kilo moja ya maua makavu ya pareto huuzwa kati ya TZS 4,000 na TZS 5,000, kutegemeana na ubora, huku uzalishaji kwa kutumia mbinu bora ukiweza kufikia hadi kilo 500 kwa ekari kwa msimu.





**Pyrethrum Processing Factory**

Hata hivyo, kuongeza uzalishaji pekee hakutoshi kufikia fursa iliyopo. Tija, upatikanaji wa mbegu bora, maarifa ya kitaalamu na usimamizi sahihi baada ya mavuno ni muhimu katika kuhakikisha ongezeko la uzalishaji linatoa malighafi yenye ubora unaohitajika na wachakataji na kuongeza thamani inayopatikana kwa wazalishaji.

COPRA inaunga mkono maendeleo ya mnyororo huu kupitia hatua mbalimbali. Mbegu bora za pareto zimesambazwa kwa wakulima, huku vituo 150 vya kukaushia pareto vikiwa vimeanzishwa katika maeneo muhimu ya uzalishaji ili kuboresha usimamizi baada ya mavuno na kuhifadhi ubora wa maua.

Ukaushaji ni hatua muhimu katika mnyororo wa thamani wa pareto kwa sababu ubora wa maua yaliyokaushwa na kiwango cha pyrethrins kilichomo huathiri thamani ya zao hilo kibiashara. Ukaushaji bora, kwa hiyo, unaimarisha uhusiano kati ya ubora unaozalishwa na mkulima na mahitaji ya wachakataji.

Pengo lililopo kati ya uzalishaji na mahitaji pia linafungua nafasi ya kuimarisha uhusiano kati ya wazalishaji na wachakataji. Kuongezeka kwa uzalishaji wa ndani kwa kiwango na ubora unaohitajika kunaweza kuwawezesha wachakataji kupata malighafi zaidi nchini, huku wakulima wakinufaika na soko ambalo tayari lina mahitaji.

"Fursa iliyopo si kuongeza uzalishaji wa pareto pekee. Tunahitaji mnyororo wa thamani ambao wakulima wanaweza kuzalisha kwa kuzingatia mahitaji ya soko, wachakataji wanapata malighafi ya uhakika na uwekezaji unaongeza thamani zaidi ndani ya Tanzania," anasema Bi. Mpinga.

Kadiri uzalishaji unavyopanuka, fursa pia zinaongezeka katika uzalishaji wa mbegu, ukusanyaji wa mazao, ukaushaji, usafirishaji, uchakataji na huduma nyingine zinazohudumia mnyororo wa thamani. Ushiriki mkubwa zaidi wa sekta binafsi katika maeneo haya unaweza kusaidia kupunguza pengo la uzalishaji na mahitaji, huku ukichochea biashara na ajira katika maeneo yanayozalisha pareto.

Wakati wachakataji wakihitaji takribani tani 9,000 kwa mwaka dhidi ya uzalishaji wa sasa wa takribani tani 4,000, soko tayari linaonesha ukubwa wa fursa iliyopo. Kupunguza pengo hili kutategemea kuongeza uzalishaji na tija, kuimarisha ubora na kujenga mifumo imara inayowaunganisha wazalishaji na wachakataji.

Kwa Tanzania, fursa ni kugeuza mahitaji ambayo bado hayajafikiwa kuwa uzalishaji zaidi, uchakataji wenye nguvu, uwekezaji mpya na thamani kubwa zaidi inayobaki nchini.



## KAKAO: FURSA MPYA YA THAMANI

# Ubora, ufuatiliaji na masoko yenye thamani zaidi

Kakao inazidi kujijengea nafasi kama zao lenye umuhimu wa kibiashara nchini Tanzania, huku ukuaji wa uzalishaji na fursa za mauzo ya nje ukiweka msingi wa kujenga mnyororo wa thamani wenye ushindani na uwezo wa kufikia masoko yenye thamani kubwa zaidi.

Katika mwaka 2024/25, Tanzania ilisafirisha nje tani 15,151.9 za kakao zenye thamani ya TZS bilioni 349.15, ikionesha thamani kubwa ya kibiashara ambayo zao hili tayari linaingiza katika uchumi. Huku uzalishaji wa kitaifa ukilenga kufikia tani 80,000 ifikapo mwaka 2030, fursa iliyopo ni kujenga juu ya msingi huu kwa kuimarisha ubora, ufuatiliaji na uzingatiaji wa matakwa ya masoko, sambamba na kupanua uchakataji na uongezaji thamani.

Tanzania inaingia katika fursa hii ikiwa na msingi mzuri wa uzalishaji. Sehemu kubwa ya kakao inazalishwa na wakulima wadogo katika mazingira asilia yanayofaa kwa zao hilo. Hii ni fursa muhimu wakati ambapo wanunuzi katika masoko ya kimataifa wanazidi kuangalia si bidhaa pekee, bali pia ilikozalishwa, namna ilivyozalishwa na iwapo uzalishaji wake unazingatia matakwa ya mazingira na uendelevu.

Kwa hiyo, fursa ya kakao haiishii katika kuongeza uzalishaji na mauzo ya nje. Ni kujenga mnyororo wa thamani unaoweza kugeuza uwezo wa uzalishaji kuwa ubora, ufuatiliaji, uzingatiaji wa matakwa ya soko na thamani kubwa zaidi ya kibiashara.

**Ufuatiliaji kufungua masoko**

COPRA inaendelea kuimarisha hatua hii kupitia usajili wa kidijitali wa wakulima na utambuzi wa maeneo ya uzalishaji wa kakao kwa kutumia taarifa za kijiografia. Hatua hiyo inasaidia kujenga taarifa zinazothibitisha wazalishaji na maeneo ya uzalishaji, msingi muhimu katika kufuatilia chanzo cha kakao katika mnyororo wa thamani.

Mifumo hii inazidi kuwa muhimu kadiri masharti ya masoko makubwa ya kimataifa yanavyobadilika. Kanuni ya Umoja wa Ulaya kuhusu bidhaa zisizochangia uharibifu wa misitu (European Union Deforestation Regulation-EUDR), inaweka masharti ya ufuatiliaji na uhakiki wa kina kwa bidhaa mbalimbali zinazoingia katika soko la Umoja wa Ulaya, ikiwemo kakao. Hivyo, taarifa sahihi za maeneo ya uzalishaji na uwezo wa kuthibitisha chanzo cha zao vinakuwa sehemu muhimu ya maandalizi ya kufikia na kuendelea kushindana katika masoko hayo.

Kupitia usajili wa wakulima na ukusanyaji wa taarifa za kijiografia za maeneo ya uzalishaji kupitia mfumo wa majira nukta na mfumo wa kidijiti wa COPRA MIS, COPRA inaweka msingi wa minyororo ya thamani inayofuatilika na kusaidia sekta ya kakao kujiandaa kukidhi matakwa yanayoibuka katika biashara ya kimataifa.

Thamani ya taarifa hizi haiishii kwenye uzingatiaji wa masharti ya masoko. Taarifa bora kuhusu wazalishaji na maeneo ya uzalishaji zinaweza kusaidia kuelekeza huduma za kitaalamu kulingana na mahitaji, kuboresha mipango na kuwapa wanunuzi uelewa mpana zaidi wa chanzo na mwenendo wa zao katika mnyororo wa thamani. Kwa mkulima, ufuatiliaji unaimarisha kiungo kati ya uzalishaji na masoko yanayozidi kuhitaji uthibitisho wa chanzo, ubora na uzalishaji unaowajibika.

**Ubora katika mnyororo wa thamani**

Sambamba na ufuatiliaji, ubora unaendelea kupewa kipaumbele. COPRA inawezesha upatikanaji wa miche bora ya kakao na kuhamasisha mbinu endelevu za uzalishaji, huku uwekezaji katika miundombinu ya baada ya mavuno ukilenga kulinda ubora wa zao kabla halijafika sokoni.

Vituo saba vya kukaushia kakao katika mikoa ya Mbeya, Morogoro na Tanga vinasaidia kuboresha usimamizi wa zao baada ya mavuno. Ukaushaji bora ni hatua muhimu katika kuhifadhi ubora na kuongeza thamani ya kibiashara ya kakao inayofikishwa sokoni.

Kwa zao ambalo ushindani wake unazidi kutegemea ubora na uwezo wa kuthibitisha chanzo chake, kuunganisha uzalishaji bora, usimamizi baada ya mavuno na ufuatiliaji kunajenga msingi imara zaidi wa kufikia masoko yenye mahitaji na thamani ya juu.

**Fursa ya uongezaji thamani**

Hatua inayofuata ni kuongeza thamani inayopatikana katika kila hatua ya mnyororo wa kakao.
Uwekezaji zaidi katika uchachushaji, ukaushaji, upangaji wa madaraja, uchakataji, ufungashaji na utengenezaji wa bidhaa zitokanazo na kakao unaweza kuongeza sehemu ya thamani inayobaki nchini. Badala ya kutegemea zaidi biashara ya zao ghafi, kupanua uwezo wa uchakataji kunaweza kufungua biashara mpya, kuongeza ajira na kupanua masoko ya bidhaa zitokanazo na kakao.



Mwelekeo huu unaendana na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, inayoweka tija, ushindani, uongezaji thamani na maendeleo ya viwanda miongoni mwa nguzo za mageuzi ya uchumi. Kwa kakao, hii inamaanisha kujenga mnyororo wa thamani unaoshindana kupitia ubora, ufuatiliaji, uzingatiaji wa matakwa ya masoko, uchakataji na uwezo wa kufikia masoko yenye thamani kubwa zaidi.

Tanzania ina uwezo wa kuongeza uzalishaji na kupanua mauzo ya kakao. Hatua inayofuata ni kugeuza uwezo huo kuwa mnyororo unaofuatilika kutoka shambani hadi sokoni, unaoweza kukidhi mahitaji yanayobadilika ya biashara ya kimataifa na unaozalisha thamani kubwa zaidi ndani ya nchi.

Kwa hiyo, mafanikio ya kakao hayatapimwa tu kwa tani zinazozalishwa na kusafirishwa nje ya nchi, bali pia kwa thamani inayojengwa na kubaki nchini kutoka katika kila punje ya kakao.



# Kuimarisha mnyororo wa thamani wenye ushindani na ustahimilivu



COPRA inachukua hatua mpya ya maendeleo ikiwa na ajenda ya miaka mitano inayolenga kuimarisha minyororo ya thamani ya nafaka na mazao mchanganyiko, kupanua fursa za kibiashara na kuongeza mchango wa sekta katika usalama wa chakula na ukuaji wa uchumi wa Tanzania.

Kupitia Mpango Mkakati wa mwaka 2026/27 hadi 2030/31, Mamlaka inalenga kujenga juu ya mafanikio yaliyopatikana katika kuimarisha mifumo ya masoko, huduma za kidijitali, uwekezaji na usimamizi wa sekta. Mwelekeo wake ni kujenga minyororo ya thamani yenye tija zaidi, iliyorasimishwa na inayounganisha uzalishaji na mahitaji ya soko.

Kipaumbele kitaendelea kuwa kuimarisha masoko yaliyorasimishwa na yenye ushindani, yanayowawezesha wazalishaji kuunganishwa kwa karibu zaidi na wanunuzi, wachakataji, taasisi za fedha na taarifa za masoko. Hii itasaidia kujenga mazingira ambayo uzalishaji unaongozwa na mahitaji ya soko na kuwawezesha wakulima kuona kilimo kama biashara yenye tija na ushindani.

Katika kipindi hicho, COPRA itaendelea kuweka mkazo katika kulinda na kuongeza thamani ya mazao yanayozalishwa. Kuboresha usimamizi baada ya mavuno, ukusanyaji wa mazao, uhifadhi, uchakataji na mifumo ya ubora kutapunguza upotevu wa mazao na kufungua fursa zaidi za uongezaji thamani na maendeleo ya viwanda vinavyotegemea mazao ya kilimo.

Mageuzi ya kidijitali yataendelea kuwa nguzo muhimu ya safari hiyo. Kupitia COPRA MIS, mifumo ya biashara ya kidijitali, huduma za kielektroniki na matumizi ya taarifa katika kufanya maamuzi, Mamlaka itaendelea kuimarisha ufuatiliaji wa minyororo ya thamani, uzingatiaji wa sheria na kanuni, pamoja na utoaji wa huduma unaozingatia mahitaji ya wadau.



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA) Bi. Irene Mlola (katikati) akichangia mada wakati wa majadiliano ya wadau kwenye Mkutano wa Kimataifa wa chakula uliofanyika Dubai, Falme za Kiarabu.


Kadiri fursa za masoko ya ndani, kikanda na kimataifa zinavyoendelea kupanuka, ushindani utaendelea kutegemea ubora, uthabiti wa uzalishaji, ufuatiliaji wa mazao na uwezo wa kukidhi matakwa ya wanunuzi. COPRA itaendelea kuimarisha viwango, mifumo ya usimamizi na uhusiano wa masoko ili kuwasaidia wazalishaji na wafanyabiashara kutumia kikamilifu fursa zinazojitokeza.

Mafanikio ya mwelekeo huu yatahitaji ushiriki wa wadau wote katika mnyororo wa thamani. Wakulima, vyama vya ushirika, wafanyabiashara, wachakataji, waendeshaji wa maghala, wasafirishaji, taasisi za fedha, wawekezaji, washirika wa maendeleo na taasisi za Serikali wote wana nafasi muhimu katika kujenga sekta yenye ushindani na ustahimilivu. Vilevile, Mamlaka itaendelea kuweka mazingira yanayopanua ushiriki wa wanawake na vijana katika uzalishaji, huduma, uchakataji, biashara na uwekezaji.

Ili kutekeleza ajenda hiyo kwa ufanisi, COPRA itaendelea kuimarisha uwezo wake wa kiutendaji kupitia maboresho ya mfumo wa kisheria, maendeleo ya rasilimali watu, usimamizi wa fedha, mifumo ya kidijitali na usimamizi wa utendaji, ili kuwa Mamlaka inayotoa huduma kwa ufanisi zaidi na inayokidhi mahitaji ya sekta inayozidi kukua.

Ifikapo mwaka 2031, matarajio ni kuwa minyororo ya thamani ya nafaka na mazao mchanganyiko itakuwa imeimarika zaidi, ikiwa na uzalishaji wenye tija, masoko yaliyorasimishwa, upotevu mdogo baada ya mavuno, uchakataji mkubwa zaidi na ushiriki mpana wa wazalishaji na wafanyabiashara katika masoko yenye ushindani.

Kwa msingi huo, safari ya COPRA inaendelea kuelekea kujenga mfumo wa chakula unaozalisha thamani zaidi, unaoimarisha usalama wa chakula, unaochochea uwekezaji na biashara, na unaochangia ukuaji jumuishi wa uchumi wa Tanzania, sambamba na maono ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.


mmoja anasoma Sheria, wapili Uchumi
wa tatu Udaktari na yupo mwingine
anaenda kusoma Biashara,"
Shukurani kubwa kwa Copra
Copra_tz
Info@copra.go.tz
www.copra.go.tz
Shirikisha,
Boresha,
Endeleza.
Toll Free
0800 11 77 77


kusomesha wajukuu na kulipa gharama
nyingine zote za maisha. Kama
nisingekuwa nalima, maisha yangu
yasingekuwa kama yalivyo sasa,"
Copra_tz
Info@copra.go.tz
www.copra.go.tz
Shirikisha,
Boresha,
Endeleza.
PIGA BURE
0800 11 77 77

- MAZAO
- MASOKO
- BIASHARA
- FURSA







## > TAMBUA SOKO
## > ONGEZA TIJA
## > JENGA BIASHARA





# MTANDAO WA OFISI ZETU




## Ufunguo wa Ramani

- Kanda ya Kati
- Kanda ya Magharibi
- Kanda ya Ziwa
- Kanda ya Kaskazini
- Kanda ya Mashariki
- Kanda ya Kusini
- Kanda ya Nyanda za Juu Kusini
- Makao Makuu
- Ofisi ya Kanda

# Habari katika picha




Aliyekuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Majaliwa Kassim Majaliwa akimkabidhi Mkurugenzi Mkuu wa COPRA Bi. Irene Mlola zawadi ya Mshindi wa kwanza kwenye maonesho ya Wiki ya CHakula Duniani yaliyofanyika jijini Tanga



Waziri wa Kilimo Mhe. Daniel Chongolo akibadilishana mawazo na watu mbalimbali akiwemo Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Bw. Gerald Mweli, Naibu Katibu Mkuu (Maendeleo ya mazao na usalama wa chakula) Prof. Peter Msoffe mara baada ya kusoma bajeti ya wizara bungeni Jijini Dodoma.




Mkuu wa COPRA Kanda ya Mashariki akiwa na wfanyakazi wa kanda hiyo kwenye maonesho ya kimataifa ya Sabasaba ambako COPRA imeshiriki kuwafikishia wananchi taarifa na huduma zinazotekelezwa na Mamlaka hiyo.

# Habari katika picha




Waziri Mkuu, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Kilimo, Mhe. Daniel Chongolo, pamoja na wadau wa sekta ya mazao ya bustani ( horticulture) wakati wa uzinduzi wa Maonyesho ya HortiLogistica Africa, yanayotarajiwa kufanyika Arusha mwezi Novemba mwaka huu.



Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Judith Kapinga akiwa kwenye maadhimisho ya Miaka 20 ya Bodi ya Usimamizi wa Maghala (WRRB), kulia kwake ni Mkurugenzi Mkuu wa Bodi hiyo Bw. Asangye Bangu. COPRA kama mdau wa bodi hiyo ilishiriki maonesho na maadhimisho hayo.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora Mhe. Ridhiwani Kikwete (MB) akisikiliza maelezo ya shughuli zinazotekelezwa na COPRA kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa COPRA Bi. Irine Mlola kwenye maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika kwenye viwanja vya Chinangali jijini Dodoma.



Naibu Waziri wa Wizara ya Kilimo Mhe. David Silinde akikabidhi cheti cha ushiriki wa COPRA kwenye maonesho ya Wiki ya Afya ya Mimea iliyofanyika kwenye viwanja vya Nanenane jijini Dodoma.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo Bw. Gerald mweli akiwa kwenye picha ya pamoja na viongozi wa Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara ya Kilimo nje ya ukumbi wa bunge baada ya kusomwa hotuba ya bajeti ya Wizara ya Kilimo.



Timu ya COPRA yashiriki Maonesho ya Nanenane, ikiendeleza dhamira ya kuimarisha ushindani, uwazi na ufanisi wa masoko ya mazao kwa maendeleo endelevu ya sekta ya kilimo Tanzania.








Waziri wa Kilimo Mhe. Daniel Chongolo (MB) akikata utepe kuzindua miongozo ya mazao ya mbaazi, ufuta na dengu akishuhudiwa na Mkuu wa Mkoa wa Lindi Mhe. Zainabu Telak, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo (anayeshughulikia umwagiliaji na zana za kilimo) Ndg. Athumani Kilundumya, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa COPRA Prof. Sifuni Mchome na Mkurugenzi Mkuu wa COPRA Bi. Irine Mlola



Washiriki wa Mkutano Mkuu wa Wadau wa Mazao wakiwa katika picha ya pamoja baada ya kikao kilicholenga kujadili mikakati ya kuimarisha uzalishaji, biashara na ushindani wa mazao nchini kupitia ushirikiano kati ya COPRA na wadau mbalimbali wa sekta ya kilimo.




Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA) Prof. Sifuni Mchome akiwa na baadhi ya wafanyakazi wa Mamlaka kwenye banda la maonesho la COPRA kwenye maonesho ya Nanenane mwaka 2025 alipotembelea kuona shughuli zinazofanyika.

*Mwaka huu naona nitapata mabadiliko makubwa sana kwasababu mwaka uliopita niliuza kilo 439 mwaka huu nategemea kuzidisha kutokana na nilichopata kwenye hii mbegu*

**Shukurani kubwa kwa Copra**




Copra_tz | Info@copra.go.tz | www.copra.go.tz

**Shirikisha, Boresha, Endeleza.**

**Toll Free 0800 11 77 77**

*Lindi White tuliyopatiwa na COPRA ina uwezo mkubwa wa kuzaa, inaonekana kustahimili changamoto za mabadiliko ya tabianchi na baadhi ya magonjwa yanayoathiri zao la ufuta.*

**Abdurahman Mohammed**

Mkulima wa Ufuta



Copra_tz | Info@copra.go.tz | www.copra.go.tz

**Shirikisha, Boresha, Endeleza.**

**Toll Free 0800 11 77 77**

# Je, Huna Account?

**1** **Bofya sehemu ilipoandikwa;**

**" I don't have an account"**

**2** **Jaza taarifa zako kwa ufasaha.**

Hakikisha taarifa zako ni sahihi kabla hujaendelea.

**3** **Kisha**

**"Create Account"**

**Anza kutumia Account.**





Tembelea
portal.copra.go.tz
Kisha Fuata Maelekezo

COPRA MIS App
Pakua App yetu sasa!




# Taarifa Muhimu Wakati wa Kutengeneza Account


**Muhimu:** Hakikisha taarifa zako ni sahihi kama zilivyoandikwa kwenye NIDA yako.

**1** **Majina Kamili (Matatu)**

**2** **Barua pepe (Email)**

**3** **Namba ya Simu** (Inayopatikana)

**3** **Namba ya NIDA**





Tembelea
portal.copra.go.tz
Kisha Fuata Maelekezo


COPRA MIS App
Pakua App yetu sasa!

# Je, Umesahau Password?

**Muhimu:** Iwapo Umesahau Nenosiri (Password)

1. **Bofya sehemu ilipoandikwa;** " **Forgot Password**"
2. **Weka namba ya simu** au **barua-pepe** uliyosajilia akaunti.
3. **Utapokea nenosiri jipya.**

**Endelea kutumia Account.**




**Tembelea**
**portal.copra.go.tz**
Kisha Fuata Maelekezo

**COPRA MIS App**
Pakua App yetu sasa!

Google Play
App Store



# WIGO WA MAZAO:

## Makundi Matano ya Kimkakati



MAMLAKA YA UDHIBITI WA NAFAKA NA MAZAO MCHANGANYIKO

COPRA

CEREALS AND OTHER PRODUCE REGULATORY AUTHORITY

## Shirikisha

Kutumia mifumo shirikishi kuratibu wadau wa nafaka na mazao mchanganyiko waliopo na wajao

## Boresha

Kuboresha minyororo ya thamani ili kuimarisha usalama wa chakula na uhakika wa masoko kwa bidhaa za nafaka na mazao mchanganyiko

## Endeleza

Kuhakikisha ongezeko la tija na uzalishaji ili kuimarisha ushindani katika soko na usalama wa chakula hatimaye kuleta maendeleo katika kipato na Maisha.

## MAWASILIANO:

Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko.

Jengo la Kahawa
Barabara ya Kahawa
S.LP 2780
Dodoma, Tanzania.

Copra_tz

PIGA BURE
0800 11 77 77

info@copra.go.tz
www.copra.go.tz

Google Play
App Store
COPRA MIS App
Pakua App yetu sasa!